# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

*(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)*

**Sehemu ya CXXXV Nam.7118** **30 June, 2023** **Bei, Shs. 3,000/=**

*Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti*

## SHERIA YA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YAUMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

### MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Marekebisho ya sheria mbali mbali.

### SEHEMU YA PILI
### MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTARATIBU NA USIMAMIZI WA KODI, NAM. 7 YA 2009

3. Kusomwa.
4. Kuongeza kifungu kipya cha 18A.
5. Marekebisho ya kifungu cha 19.
6. Kuongeza vifungu vipya vya 19A, 19B na 19C.
7. Marekebisho ya kifungu cha 20.
8. Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 21.
9. Marekebisho ya kifungu cha 21B.
10. Marekebisho ya kifungu cha 23.
11. Marekebisho ya kifungu cha 31.
12. Marekebisho ya kifungu cha 33.
13. Marekebisho ya kifungu cha 59.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjika kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanawezakutiwakatikaGazeti.Nakalamatangazonamnahiyo,zipelekwekwaMhaririwaGazetiRasmilaSerikaliyaMapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga, Sanduku la Posta 261. Nakala zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

Scanned with CamScanner

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA 1998**

14. Kusomwa.
15. Marekebisho ya kifungu cha 8.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA MAJENGO, NAM. 14 YA 2008**

16. Kusomwa.
17. Marekebisho ya kifungu cha 28.

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA STEMPU, NAM. 7 YA 2017**

18. Kusomwa.
19. Marekebisho ya kifungu cha 3.
20. Marekebisho ya kifungu cha 60.
21. Kufuta kifungu cha 62

**SEHEMU YA SITA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAFIRI BARABARANI, NAM. 7 YA 2003**

22. Kusomwa.
23. Marekebisho ya kifungu cha 2.

**SEHEMU YA SABA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAFUNZO YA AMALI, NAM. 8 YA 2006**

24. Kusomwa.
25. Marekebisho ya kifungu cha 27.

**SEHEMU YA NANE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA (USIMAMIZI WA MAPATO YA UMMA), NAM. 9 YA 2015**

26. Kusomwa.
27. Marekebisho ya kifungu cha 20.
28. Kuongeza kifungu kipya cha 20A.

Scanned with CamScanner

**SHERIA NAM. 3 YA 2023**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

**23 Juni, 2023**

# SHERIA YA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2023 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti Rasmi. Jina fupi na kuanza kutumika.

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika. Marekebisho ya sheria mbali mbali.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTARATIBU NA USIMAMIZI WA KODI, NAM. 7 YA 2009

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, Nam. 7 ya 2009 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama". Kusomwa.

**4.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 18A mara baada ya kifungu cha 18 kama ifuatavyo: Kuongeza kifungu kipya cha 18A.

> **18A.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza kumuagiza mlipa kodi kuwasilisha ritani ya kodi tarehe ya mapema kabla ya tarehe iliyoainishwa katika kifungu cha 18 cha Sheria hii, ikiwa mlipa kodi:
>
> (a) anataka kuondoka Zanzibar moja kwa moja;
>
> (b) anataka kufunga biashara moja kwa moja; au
>
> (c) amefilisika, anaelekea kufilisika au amevunja kampuni.

Scanned with CamScanner

(2) Maagizo ya Kamishna Mkuu chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, yatakuwa kwa maandishi na yatawasilishwa kwa mlipa kodi yakiainisha kipindi au taarifa itakayojumuishwa katika ritani ya kodi na tarehe ya kuwasilisha ritani ya kodi."

Marekebisho ya kifungu cha 19.

**5.** Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (1), kufuta maneno "faini, adhabu na" yaliyopo baina ya maneno "kutoza" na "riba"; na

(b) katika kifungu kidogo cha (3), kufuta maneno "faini, adhabu na" yaliyopo baina ya maneno "yoyote" na "riba".

Kuongeza vifungu vipya vya 19A, 19B na 19C.

**6.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza vifungu vipya vya 19A, 19B na 19C mara baada ya kifungu cha 19 kama ifuatavyo:

**19A.**-(1) Endapo mlipa kodi anatakiwa kuwasilisha ritani chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote ya kodi, ritani ya kodi itakayowasilishwa itakuwa ni tathmini binafsi ya deni la kodi.

(2) Mtu asiyekuwa Kamishna Mkuu hatarekebisha au kufanya mabadiliko ya tathmini chini ya kifungu hiki.

**19B.**-(1) Kamishna Mkuu anaweza wakati wowote kufanya tathmini ya lazima endapo mlipa kodi ameshindwa kuwasilisha ritani ya kodi katika tarehe ya mwisho ya kuwasilisha ritani.

(2) Kamishna Mkuu anaweza kutumia uamuzi unaofaa na taarifa zilizopatikana katika kufanya tathmini ya lazima.

(3) Tathmini ya lazima haitomuondoshea mlipa kodi wajibu wa kuwasilisha ritani ya kodi.

(4) Uwasilishaji wa ritani ya kodi hautoathiri tathmini ya lazima.

(5) Tathmini ya lazima inaweza kuwa halali kwa kipindi kuhusiana na tukio au jambo linalohusika kama Kamishna Mkuu atakavyoainisha katika taarifa ya tathmini.

(6) Endapo tathmini ya lazima itajumuisha kipindi au jambo lililojumuishwa katika tathmini binafsi ya mlipa kodi kuhusiana na kodi hiyo, kodi yoyote iliyolipwa kuhusiana na tathmini ya lazima itakuwa ni deni la kodi inayolipwa kuhusiana na tathmini binafsi.

Scanned with CamScanner

**19C.-(1)** Kamishna Mkuu anaweza, hata kama hakuna pingamizi au rufaa ya kodi iliyowasilishwa, kuondoa tathmini iliyotolewa ikiwa amejiridhisha kuwa tathmini ilitolewa:

(a) kwa mlipa kodi asiyekuwa sahihi;

(b) kuhusiana na kipindi cha kodi kisichokuwa sahihi;

(c) kutokana na kutokuwa sahihi kwa wigo wa kodi, kiwango, taarifa au hesabu; na

(d) kwa sababu nyengine yoyote ya kisheria itakayopelekea tathmini hiyo kuondolewa.

(2) Tathmini iliyoondolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itachukuliwa kuwa haijatolewa."

**7.** Kifungu cha 20 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika aya ya (c) kwa kufuta maneno "faini, adhabu " yaliyopo baina ya maneno "kiwango" na "riba". Marekebisho ya kifungu cha 20.

**8.** Kifungu cha 21 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa badala yake kifungu kipya cha 21 kama ifuatavyo: Kufuta na kuweka badala yake kifungu cha 21.

**21.** Taarifa ya tathmini iliyotolewa chini ya Sheria hii itawasilishwa kwa mlipa kodi aliyefanyiwa tathmini na kumjuilisha haki yake ya pingamizi chini ya masharti ya Sheria hii.

**9.** Kifungu cha 21B cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa: Marekebisho ya kifungu cha 21B.

(a) kufuta vifungu vidogo vya (3) na (5) na kuweka badala yake vifungu vidogo vipya vya (3) na (5) kama ifuatavyo:

"(3) Endapo Kamishna Mkuu atakubali kurekebisha uamuzi au tathmini iliyowekewa pingamizi, uamuzi au tathmini hiyo itarekebishwa ipasavyo na Kamishna Mkuu atatoa taarifa inayoainisha marekebisho ya uamuzi au tathmini iliyowekewa pingamizi na kuiwasilisha kwa mtu huyo.

(5) Endapo Kamishna Mkuu:

(a) anakusudia kurekebisha uamuzi au tathmini iliyowekewa pingamizi kwa mujibu wa pingamizi na ushahidi wowote wa ziada; au

(b) anaamua kukataa kurekebisha uamuzi au tathmini iliyowekewa pingamizi,atampa taarifa mtu aliyeweka pingamizi inayoelezea sababu ya kusudio au uamuzi wake.

Scanned with CamScanner

(b) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (6) na (7) mara baada ya kifungu kidogo cha (5) kama ifuatavyo:

"(6) Mtu aliyeweka pingamizi, ndani ya siku ishirini na moja kutoka siku ya kupokea taarifa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, atawasilisha kwa maandishi kwa Kamishna Mkuu kueleza kukubaliana au kutokubaliana na marekebisho ya uamuzi au tathmini iliyowekewa pingamizi au kukataa.

(7) Kamishna Mkuu anaweza, baada ya kumalizika kwa siku ishirini na moja za kuwasilisha taarifa kwa mtu alioweka pingamizi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (6) cha kifungu hiki:

(a) kuamua pingamizi kulingana na marekebisho ya uamuzi au tathmini iliyowekewa pingamizi au kukataa na uwasilishaji wowote wa mtu aliyeweka pingamizi; au

(b) kuamua sehemu ya pingamizi kwa mujibu wa uwasilishaji wa mtu aliyeweka pingamizi, na kuendelea kutoa uamuzi wa mwisho wa pingamizi".

Marekebisho ya kifungu cha 23.

**10.** Kifungu cha 23 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mlipa kodi anayetoa risiti iliyoidhinishwa kupitia mfumo wa malipo ya kielektroniki ya Serikali atahesabika kuwa ametoa risiti kwa kutumia mashine ya kielektroniki ya kutolea risiti".

(b) kuvipa nambari upya vifungu vidogo vya (2), (3), (4), (5) na (6) kuwa vifungu vidogo vipya vya (3), (4), (5), (6) na (7) kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 31.

**11.** Kifungu cha 31 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (3).

Marekebisho ya kifungu cha 33.

**12.** Kifungu cha 33 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta neno "tano" linalojitokeza katika kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake neno "kumi".

Marekebisho ya kifungu cha 59.

**13.** Kifungu cha 59 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (2) kwa kuongezwa aya mpya ya (d) kama ifuatavyo:

(d) kuondoa tathmini.

Scanned with CamScanner

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA 1998

**14.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya 1998 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama". Kusomwa.

**15.** Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuingiza maneno "isipokuwa kwa huduma za benki, posta na mawasiliano ambapo kiwango cha kutozea kodi kitakuwa asilimia kumi na nane" mwishoni mwa kifungu hicho. Marekebisho ya kifungu cha 8.

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA MAJENGO, NAM. 14 YA 2008

**16.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Majengo, Nam. 14 ya 2008 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama". Kusomwa.

**17.** Kifungu cha 28 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufuta aya ya (a). Marekebisho ya kifungu cha 28.

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USHURU WA STEMPU, NAM. 7 YA 2017

**18.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ushuru wa Stempu, Nam. 7 ya 2017 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama". Kusomwa.

**19.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa: Marekebisho ya kifungu cha 3.

(a) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Ushuru wa Stempu katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utatozwa na kukusanywa:

(a) kwa hati zote kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Jadweli la Kwanza la Sheria hii, isipokuwa kwa hati zilizoanishwa kusamehewa kulipiwa ushuru huo; au

(b) kwa mauzo ghafi ya usambazaji wa bidhaa na huduma kwa walipakodi wadogo na kati ambayo yatatozwa katika kiwango kilichoainishwa chini ya Jadweli la Pili, la Tatu na la Nne la Sheria hii."

(b) kufuta vifungu vidogo vya (3), (4), (5) na (6).

**20.** Kifungu cha 60 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo: Marekebisho ya kifungu cha 60.

Scanned with CamScanner

"(2) Waziri anaweza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, kurekebisha, kubadilisha au kuweka upya Jadweli lolote chini ya Sheria hii."

Kufuta kifungu cha 62

**21.** Kifungu cha 62 cha Sheria Mama kinafutwa.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USAFIRI BARABARANI, NAM. 7 YA 2003

Kusomwa.

**22.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usafiri Barabarani, Nam. 7 ya 2003 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**23.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza maneno "au 2238W ~ 2.23KW" baina ya maneno "isiyozidi 50cc" na neno "na" katika tafsiri ya neno "mopedi".

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAFUNZO YA AMALI, NAM. 8 YA 2006

Kusomwa.

**24.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mafunzo ya Amali, Nam. 8 ya 2006 ambapo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**25.** Kifungu cha 27 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (2), kufuta neno "nne" na kuweka badala yake neno "tano";

(b) katika kifungu kidogo cha (3), kufuta maneno "asilimia tano (5%)" na kuweka badala yake maneno "asilimia nne"; na

(c) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (8) na (9) mara baada ya kifungu kidogo cha (7) kama ifuatavyo:

"(8) Mwajiri mwenye waajiriwa watatu au wasiozidi watano atatakiwa kuwasilisha ritani isiyokuwa na kitu kila baada ya miezi sita kupitia mfumo wa kielektroniki wa uwasilishaji au njia yoyote ile itakayoainishwa na Naibu Kamishna.

(9) Kwa kuzingatia masharti chini ya kifungu kidogo cha (8) cha kifungu hiki, endapo mwajiri atashindwa kuwasilisha ritani ya kila baada ya miezi sita, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano za Kitanzania"

Scanned with CamScanner

## SEHEMU YA NANE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA FEDHA (USIMAMIZI WA MAPATO YA UMMA), NAM. 9 YA 2015

**26.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), Nam. 9 ya 2015 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama". Kusomwa.

**27.** Kifungu cha 20 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (6) na (7). Marekebisho ya kifungu cha 20.

**28.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 20A mara baada ya kifungu cha 20 kama ifuatavyo: Kuongeza kifungu kipya cha 20A.

**20A.**-(1) Viwango vinavyotozwa chini ya kifungu cha 20(3) cha Sheria hii, vinavyohusiana na uingizaji wa bidhaa isipokua kwa bidhaa za mafuta, vilevi, sigara na tumbuku havitotumika kwa:

(a) Taasisi za Serikali ambazo hazitengenezi faida na zinazofadhiliwa chini ya Mfuko Mkuu wa Hazina, Miradi ya Washirika wa Maendeleo, Mabalozi au Ujumbe wa Mabalozi, Umoja wa Mataifa na Mashirika yake; na

(b) malighafi, pembejeo za viwandani na vifungashio kwa wazalishaji waliosajiliwa.

(2) Kwa madhumuni ya kifungu hiki "Mabalozi au Ujumbe wa Mabalozi" ni wale wote walioanishwa chini ya Jadweli la Tatu la Sheria ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya 1998".

**IMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 21 Juni, 2023.

(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***

Scanned with CamScanner